Tangazo la Serikali Namba 445 la Tarehe 7 Novemba 2014

SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA

SURA YA 290.

SHERIA NDOGO.

Zimetungwa chini ya kifungu vya 7(1) (i)).

SHERIA NDOGO ZA (ADA YA LESENI ZA BIASHARA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA LUDEWA, 2014.

Jina na tarehe ya kuanza kutumika.

1 Sheria hizi zitajulikana kama Sheria ndogo za (Ada ya Leseni za Biashara**)** za Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa, 2014. Na zitaanza kutumika mara baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Eneo la kutumika

2 Sheria ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililoko ndani ya Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa.

Tafsiri.

3 Katika Sheria ndogo hizi, isipokuwa ikielezwa vinginevyo.

‘Ada’ maana yake ni malipo yanayolipwa kwa halmashauri kwa ajili ya leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri.

‘Afisa Mwidhiniwa’ maana yake ni mtumishi wa Halmashauri aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa sheria ndogo hizi.

‘Biashara’ maana yake ni shughuli yoyote ya kubadilisha bidhaa, uchuuzi, kuzalisha au kutengeneza bidhaa, kutoa au kutumia huduma kwa lengo la faida au kupata kipato.

‘Biashara ya jumla’ maana yake ni biashara inayohusisha kuuza bidhaa kwa mchuuzi ambaye naye atauza bidhaa hiyo kwa mlaji.

‘Biashara” ya rejareja’ maana yake ni biashara inayohusisha kuuza bidhaa moja kwa moja kwa mlaji.

‘Biashara za utaalam maalum’ maana yake ni shughuli za kitaalam kama vile udaktari, washauri nasaa, wanasheria, wakaguzi wa mahesabu, washauri wa kodi, washauri wa biashara na nyinginezo.

‘Halmashauri’ maana yake Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa.

‘Leseni ya biashara’ maana yake ni leseni itakayotolewa kwa mujibu wa sheria ndogo hii inayomruhusu mfanyabiasara kufungua biashara yake.

‘Wakala’ maana yake ni mtu, kikundi cha watu au kampuni kilichoteuliwa na Halmashauri.

‘Mfanyabiashara’ maana yake ni mtu, kikundi, au Kampuni inayofanya biashara.

‘Mkurugenzi’ maana yake Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya Ludewa ikiwa ni pamoja na Afisa yeyote aliyeteuliwa kukaimu nafasi hiyo.

‘Mmiliki’ ni mtu mwenye biashara husika.

‘Viwanda vidogo’ maana yake ni pamoja na utengenezaji wa unga wa aina tofauti, batiki, mvinyo na vinginevyo.

‘Wakala’ maana yake ni mtu yeyote au kikundi chochote atakayeteuliwa na Halmashauri kwa maandishi kwa lengo la kukusanya ada chini ya sheria ndogo hizi.

Sura ya 290

‘Sheria” maana yake ni Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa.

Utoaji wa Leseni.

4 (1) Halmashauri itatoa leseni kwa ajili ya biashara mbalimbali zitakazofanyika ndani ya eneo la Halmashauri, baada ya mwombaji kujaza fomu maalumu ya maombi ya Leseni.

(2) Leseni za biashara zitakazotolewa chini ya Sheria ndogo hizi kila baada ya muda wa mwaka mmoja kuanzia mwezi Julai hadi mwezi Juni mwaka unaofuata.

(3) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kubadilisha viwango vya malipo ya ada ya leseni muda wowote itakavyoona inafaa na kwa mujibu wa taratibu na masharti ya sheria kadri itakavyoamriwa.

(4) Utakuwa ni wajibu wa kila mfanyabiashara kuwa na leseni halali ya biashara yake kwa mujibu wa Sheria ndogo hizi na kulipia Leseni yake kila mwaka kama ilivyoelekezwa kwenye Jedwali Na.2 la Sheria ndogo hizi.

(5) Kila mmiliki wa biashara atatakiwa kuweka leseni yake katika eneo/sehemu ya biashara yake iliyo wazi kuepuka usumbufu wakati wa ukaguzi.

Malipo ya Leseni kulipwa kwa Halmashauri.

5 (1) Malipo ya leseni yatakayotozwa chini ya Sheria ndogo hizi, yatalipwa kwa Halmashauri au wakala wake ambaye atatoa stakabadhi inayotambulika na Halmashauri kama kielelezo cha kukubali malipo hayo na kutoa leseni.

(2) Wakala atakayekusanya malipo ya leseni chini ya Sheria ndogo hizi atawajibika kuzingatia masharti na maelekezo yaliyomo katika Sheria ndogo hizi.

(3) Halmashauri inaweza kutenga vituo katika maeneo ya Halmashauri kwa ajili ya kuhudumia wananchi wanaohitaji leseni za biashara ndani ya mamlaka ya Halmashauri.

(4) Ada ya leseni italipwa mara baada ya mhusika kujaza fomu maalum na itakayotolewa na Halmashauri na kufanya uthaminishaji wa kiwango cha ada ya leseni anachotakiwa kulipa.

Muda wa malipo ya Leseni

6 (1) Malipo yote ya leseni yatalipwa kwa hiari kila tarehe moja ya Mwezi Julai ya kila mwaka hadi tarehe thelathini ya mwezi Septemba kila mwaka. Mtu yeyote atakayefanya biashara bila leseni baada ya kuisha muda huo atakuwa amekiuka Sheria Ndogo hizi na atakuwa ametenda kosa.

Ukaguzi wa leseni.

7 (1) Afisa mwidhiniwa atakuwa na mamlaka ya kuingia katika eneo lolote la biashara kukagua leseni za biashara. Ukaguzi wa leseni za biashara utafanyika muda na wakati wa saa za kazi.

Wajibu wa mfanyabi

8 (1) Kila mmiliki wa biashara anatakiwa na leseni ya biashara kabala ya kuanza biashara yake.

(2)

ashara.

(3) Kila mfanyabiashara anatakiwa baada ya muda wa leseni yake kuisha kulipa ada ya leseni kila baada kuisha muda wake.
Kila mmiliki wa biashara atatakiwa kuweka leseni yake katika sehemu ya biashara yake iliyo wazi kuepuka usumbufu wakati wa ukaguzi.

Halmashauri kutowajibika kwa hasara. 9 Halmashauri haitawajibika kwa hasara yoyote na kwa namna yoyote ile itakayotokea wakati wa ukaguzi wa leseni za biashara.

Makosa na Adhabu 12 (1) Itakuwa ni kosa kwa mujibu wa Sheria ndogo hizi endapo mtu yeyote

(a) Ataendesha biashara yake bila leseni.
(b) Ataendesha biashara tofauti na inayoelezwa kwenye leseni yake.
(c) Atatoa lugha ya matusi wakati wa zoezi la ukaguzi.
(d) Ataleta au kusababisha usumbufu wowote kwa mkaguzi wa leseni.
(e) Atachanganya biashara iliyosajiliwa kwenye leseni na nyingine isiyo kwenye leseni.
(f) Atamzuia Afisa muidhiniwa kufanya shughuli za ukaguzi.

(2) Mtu yeyote atakayekiuka au kuvunja Sheria ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi mia tatu elfu (300,000/=) au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili (12) au vyote kwa pamoja kifungo na faini.

(3) Bila kuathiri kifungu cha 12(2) cha Sheria ndogo hizi, Halmashauri itakuwa na haki ya kuendelea kudai malipo ya Ada ya Leseni yanayohitajika kwa mfanyabiashara aliyepatikana na hatia.

Mamlaka ya Mkurugenzi kufifilisha kosa

Bila kuathiri mashrti ya Sheria Ndogo hizi Mkurugenzi atakuwa na uwezo na mamlaka ya kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote faini isiyozidi shilingi mia tatu elfu (Tshs.300,000/=) pamoja na ada ya leseni inayotakiwa kulipwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi iwapo mkosaji kwa hiari yake mwenyewe atakiri kosa hilo kwa kujaza fomu maalum iliyoanishwa kwenye Jedwali Na.1 la Sheria Ndogo hizi.

Jedwali Na.1

Form Na. LDC/01/L2

Halmashauri ya Wilaya Ludewa

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji

FOMU YA KUFIFILISHA KOSA

(Chini ya Kifungu cha 16)

Mimi……wa S.L.P…….ninayefanya biashara ya …..katika eneo la ……lililopo katika eneo la Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya Ludewa, kwa hiari yangu mwenyewe nakiri kuwa tarehe……mwezi……mwaka……nilikiuka kifungu cha ……..cha Sheria Ndogo za (Ada ya Leseni za Biashara) za Halmashauri ya Wilaya Ludewa za mwaka 2012.
Kwa hiyo, kwa hiari yangu mwenyewe na bila kushurutishwa na mtu yeyote nakubali kulipa faini iliyoainishwa kwenye Sheria Ndogo hizi iwapo Mkurugenzi ataamua kutekeleza madaraka yake aliyopewa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

Saini……
Mbele yangu……..(Jina)
Saini…….
Wadhifa……..
Tarehe……

Jedwali Na. 2

SEHEMU A.

Kada za Biashara	Aina ya Biashara	Ada ya Leseni kwa mwaka. (Tshs.)
Kandarasi za Ujenzi	(i) Wajenzi wa Kawaida.	100,000
	(ii) Mkandarasi daraja I	800,000
	(iii) Mkandarasi daraja II	750,000
	(iv) Mkandarasi daraja III	700,000
	(v) Mkandarasi daraja Iv	650,000
	(vi) Mkandarasi daraja V	500,000
	(vii) Mkandarasi daraja vi	200,000
	(viii) Mkandarasi araja vii.	300,000

SEHEMU B

Kada za Biashara	Aina ya Biashara	Ada ya Leseni kwa mwaka(Tshs.)
Kandarasi za Umeme.	(i) Mkandarasi wa kawaida.	30,000 - 50,000
	(ii) Mkandarasi daraja A	300,000
	(iii) Mkandarasi daraja B	200,000
	(iv) Mkandarasi daraja C	100,000
	(v) Mkandarasi daraja D	100,000

SEHEMU C

Kada za Biashara	Aina ya Biashara	Ada ya Leseni kwa mwaka(Tshs.)
Hoteli **ada hizi zitaongezeka au kupungua kwa 20% kulingana na ukubwa wa biashara	i) Nyumba za kulala wageni.	50,000
	ii) Hoteli za kitalii.	100,000
	iii) Hoteli ya kitalii isiyo na vinywaji vikali.	80,000
	iv) Mgahawa.	20,000
	v) Hoteli ya kawaida.	50,000
	vi) Huduma ya chakula (catering services)	30,000

SEHEMU D.

Kada za Biashara	Aina ya Biashara	Ada ya Leseni kwa mwaka(Tshs.)
Mawasiliano	i. Huduma za Internet.	80,000
	ii. Maduka ya kuuza simu	100,000
	iii. Maduka ya kuuza vifaa vya simu	50,000
	iv. Usafirishaji wa abiria zaidi ya abiria 30	100,000
	v. Usafirishaji wa Abiria chini ya Abiria 30	80,000
	vi. Usafirishaji wa Abiria kwa tax	20,000
	vii. Vituo vya Redio	200,000
	viii. Huduma za posta	50,000
	ix. Usafirishaji wa mizigo.	200,000

SEHEMU E.

Kada za Biashara	Aina ya Biashara	Ada ya Leseni kwa mwaka(Tshs.)
Huduma za Afya	i) Uuzaji wa dawa kwa jumla.	100,000
	ii) Maabara	50,000
	iii) Zahanati	50,000
	iv) Duka la dawa muhimu	50,000

	v)	Hospitali	100,000
	vi)	Vifaa tiba	200,000

SEHEMU F.

Kada za Biashara	Aina ya Biashara		Ada ya Leseni kwa mwaka(Tshs.)
Kilimo	i)	Duka la pembejeo	100,000
	ii)	Duka la dawa za mifugo	100,000

SEHEMU G.

Kada za Biashara	Aina ya Biashara		Ada ya Leseni kwa mwaka(Tshs.)
Mafuta na Gesi	i)	Kituo cha mafuta (shell)	150,000
	ii)	Uuzaji wa oil na vilainisho.	100,000
	iii)	Maduka ya gesi	100,000
	iv)	Duka la mafuta ya rejareja	50,000

SEHEMU H.

Kada za Biashara	Aina ya Biashara		Ada ya Leseni kwa mwaka(Tshs.)
Biashara za Bidhaa mbalimbali ** ada hizi zitaongezeka au kupungua kwa 20% kulingana na ukubwa wa biashara	i)	Duka la jumla bidhaa mbalimbali	200,000
	ii)	Duka la reja rejea	40,000
	iii)	Duka la vipodozi	30,000
	iv)	Duka la samaki wabichi	30,000
	v)	Duka la nguo na viatu	30,000
	vi)	Saloon	30,000
	vii)	Shajala	50,000
	viii)	Maduka ya vifaa vya nyumbani	80,000
	ix)	Maduka ya samani za kigeni.	100,000
	x)	Maduka ya ushonaji na vifaa vyake	30,000
	xi)	Maduka ya radio, TV na spea zake	50,000
	xii)	Mashine ya kusaga	30,000
	xiii)	Min supermarket	50,000
	xiv)	Super market.	70,000
	xv)	Viwanda vya uselemala	30,000
	xvi)	Uuzaji wa mbao	80,000
	xvii)	Uuzaji mkaa	80,000
	xviii)	Uuzaji nafaka	50,000
	xix)	Bucha.	40,000
	xx)	Uuzaji vifaa vya Baiskeli	50,000
	xxi)	Uuzaji vifaa vya pikipiki	80,000
	xxii)	Uuzaji vifaa vya magari.	100,000
	xxiii)	Uuzaji vifaa vya ujenzi	50,000
	xxiv)	Karakana (gereji)	70,000
	xxv)	Uuzaji wa vifaa vya umeme	50,000
	xxvi)	Uuzaji wa mifugo (minada)	50,000
	xxvii)	Vioski.	10,000
	xxviii)	Studio za picha/miziki/filamu	30,000
	xxix)	Uuzaji wa vyakula mbalimbali	40,000
	xxx)	Huduma ya kufua nguo	30,000
	xxxi)	Huduma ya kupamba kumbi za harusi na sherehe mbalimbali	30,000

SEHEMU I.

Kada za Biashara	Aina ya Biashara		Ada ya Leseni kwa mwaka(Tshs.)
Viwanda	i)	Viwanda vidogo.	100,000
	ii)	Viwanda vya kati.	750,000
	iii)	Viwanda vikubwa.	1,000,000

SEHEMU J

Kada za Biashara	Aina ya Biashara	Ada ya Leseni kwa mwaka(Tshs)

Tasisi za kifedha.	i)	Huduma za kubadilisha fedha	400,000
	ii)	Taasisi za kutoa mikopo/kampuni	200,000
	iii)	Mifuko ya hifadhi ya jamii	200,000
	iv)	Bank za kijamii na SACCOS	40,000
	v)	Huduma za simu kutuma pesa (M-Pesa, T-Pesa, Airtel Money, n.k.	50,000

SEHEMU K

Kada za Biashara	Aina ya Biashara		Ada ya Leseni kwa kila mwaka.
Ufundi wa huduma nyingine	i)	Karakana.	50,000
	ii)	Studio	50,000

SEHEMU L.

Kada za Biashara	Aina ya Biashara	Ada ya Leseni kwa mwaka (Tshs.)
Elimu na ushauri mwingine wa kitaalamu	Chuo binafsi	200,000
	Shule ya bweni binafsi	100,000
	Shule ya kutwa binafsi	50,000
	Ushauri wa Biashara (Business consultancy)	100,000
	Ushauri wa Kodi (Tax consultancy)	100,000
	Upimaji wa ardhi (land surveyors)	100,000
	Ukaguzi na Uhasibu (Auditor accountants)	100,000
	Wachoraji ramani za majengo	100,000
	Ushauri wa kitabibu/Ushauri nasaha	80,000
	Ushauri wa kisheria	100,000
	Ukadiriaji majengo (quantity surveyor)	100,000
	Huduma nyingine za ushauri wa kitaalam	70,000

SEHEMU M.

Kada za Biashara	Aina ya Biashara	Ada ya Leseni kwa mwaka(Tshs.)
UDALALI	Dalali wa kuuza na kununua madini	100,000
	Dalali wa mahakama	100,000
	Dalali wa biasahra mbalimbali	50,000
	Makampuni ya matangazo(promotion)	30,000

SEHEMU N.

Kada za Biashara	Aina ya Biashara	Ada ya Leseni kwa mwaka (Tshs.)
Michezo ya kuhabatisha na sehemu za starehe	Slot mashine	100,000

SEHEMU O.

Kada za Biashara	Aina ya Biashara	Ada ya Leseni kwa mwaka (Tshs.)
Vituo vya kuuzia bidhaa za viwandani (Depots)	Mini-depots	100,000

Mhuri wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa umewekwa kwenye Sheria ndogo hizi kufuata azimio la Mkutano wa Baraza la Madiwani uliofanyika katika Ukumbi wa Halmashauri tarehe 11 mwezi Februari mwaka 2014 na kubandikwa mbele ya:-

……..
William N.Waziri
Mkurugenzi Mtendaji (W).
Halmashauri ya Wilaya Ludewa.

……
Mathei Felician Kongo
Mwenyekiti
Halmashauri ya Wilaya Ludewa.

NAKUBALI,

……
MIZENGO P. PINDA (MB)
WAZIRI MKUU.

DODOMA.

Tarehe,……